Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania


Co-funded by the European Union

USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA VIJIJI: UHIFADHI ENDELEVU, MAISHA BORA KWA JAMII HANDENI

Kijiji cha Gendagenda kimefanikiwa kuwaondoa zaidi ya watu 200 waliokuwa wakiishi ndani ya msitu wa hifadhi wa kijiji.







Usimamizi endelevu wa misitu umewezesha vijiji kupata mapato kwa ajili ya uhifadhi na maendeleo. Bank statement ikionyesha kiasi cha pesa kilichokusanywa na Kijiji cha Gendagenda. Mpaka kufikia Mwezi Februari 2026 Kijiji kilikuwa kimekusanya shilingi milioni 107 kutokana na biashara endelevu ya mazao ya misitu



Doria za misitu zimeimarisha ulinzi wa rasilimali za misitu na kudhibiti shughuli zisizoruhusiwa. Picha inaonyesha baadhi ya vifaa vilivyotaifishwa wakati wa doria katika Kijiji cha Gendagenda.


Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union


UFUGAJI NYUKI, FURSA YA KIPATO NA UJASIRIAMALI HANDENI



Picha 1: Utajiri wa msitu, fursa ya kipato! Wafugaji nyuki wa Kijiji cha Mkalamo wakirina asali, matunda ya juhudi zao katika ufugaji nyuki. Mafunzo na vifaa walivyopatiwa vimesaidia kuongeza mavuno zaidi.



Wananchi wakionyesha bidhaa zitokanazo na ufugaji nyuki zinazowaongezea kipato, kukuza ujasiriamali na kuboresha maisha yao.



Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union

VIKUNDI VYA KUWEKA NA KUKOPA VYAFUNGUA FURSA ZA KIPATO NA KUPUNGUZA UTEGEMEZI WA MISITU WILAYANI HANDENI



Picha 1: Juma Hamis Bakari, mnufaika wa VICOBA kutoka Kijiji cha Gendagenda, alitumia shilingi 700,000 kuanzisha ufugaji wa mbuzi, ambao huwauza wakati wa sikukuu ili kuongeza kipato.



Picha 2: Bwana Ramadhani Semkanda kutoka Kijiji cha Kwamsisi aeleza jinsi VICOBA ilivyomwezesha kupata mkopo nafuu wa kuchimba kisima na kununua pampu na tanki la maji. Sasa anatoa huduma ya maji kwa jamii na kupata kipato cha kutunza familia na kusomesha watoto wake.



Picha 3; VICOBA yafungua milango ya ujasiriamali. Yusuph Mnondwa Bakari, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mkalamo akionyesha mradi wake wa ufugaji kuku kama chanzo cha kipato.



Picha 4; VICOBA yajenga matumaini ya maisha bora! Bi. Mwajuma Hamisi Athumani kutoka Kijiji cha Mkalamo ametumia fursa ya VICOBA kununua kiwanja na kuanza ujenzi wa nyumba yake, akitarajia kutumia faida ya mzunguko ujao kuendeleza ujenzi huo.

Picha 5: ICOBA YAFUNGUA MILANGO YA UJASIRIAMALI! Tabu Rajabu, mnufaika wa kikundi cha VICOBA, ameanzisha duka la vinywaji na kununua friji, hatua inayomwezesha kuongeza kipato na kuboresha maisha yake na ya familia yake



Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union

USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU YA VIJIJI: KUIMARISHA USIMAMIZI WA ARDHI NA MISITU PAMOJA NA NA KUBORESHA HUDUMA ZA JAMI



1

Utatuzi wa migogoro ya mipaka kati ya Kijiji cha Lusane na vijiji jirani umeimarisha ulinzi wa msitu wa hifadhi ya kijiji, baada ya kuwaondoa wavamizi waliokuwa wamejenga makazi ndani ya msitu.



2

Misitu Yaleta Maji Safi na Salama! Mapato yatokanayo na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu katika Kijiji cha Mnkonde, Wilaya ya Kilindi, yamewezesha ujenzi na ukarabati wa kisima cha maji, kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama kwa jamii.



3

Fatuma Heli Kabelwa, mkazi wa Kijiji cha Mnkonde, akiandaa mzinga wa nyuki kwa ajili ya kuutundika katika msitu wa hifadhi ya kijiji. Uwepo wa msitu wenye miti na maua mbalimbali huwapatia nyuki chakula na mazingira bora ya kuzaliana na kuzalisha asali

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union



KUTOKA WAFUGAJI HADI VINARA WA UHIFADHI WA MISITU WILAYANI KILINDI

1 Wajumbe wa Kikundi cha Sinyati, Kijiji cha Lusane, wakikagua mizinga ya nyuki ili kuhakikisha usalama wao na kuimarisha ufugaji nyuki kama fursa ya kipato na uhifadhi wa misitu.

2 Wafugaji nyuki wa kikundi cha Sinyati Kijiji cha Lusane, wakiwa katika picha ya pamoja na waandishi wa habari waliotembelea eneo lao la ufugaji nyuki. Shughuli za ufugaji nyuki unachochea uhifadhi wa misitu na kuongeza kipato cha jamii.





3 Kupitia mradi, jamii za wafugaji zimejengewa uwezo na sasa zinashiriki kikamilifu katika kulinda misitu, huku zikifungua fursa za ufugaji nyuki na kuongeza kipato.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union


VIKUNDI VYA KUWEKA NA KUKOPA VYAWAWEZESHA WANAWAKE WAFUGAJI KUMILIKI MIFUGO



Bi. Hadija Manyagala, mkazi wa Kijiji cha Lusane, akionyesha stoo ya mahindi waliyonunua kwa ajili ya kuuza wakati wa kiangazi, ambapo uhaba wa chakula huongeza mahitaji na kuwawezesha kupata faida



Bi. Lucia Zuberi wa Kijiji cha Lusane akionyesha ng'ombe walionunuliwa na kikundi chao cha Sinyati, ishara ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.





Ushiriki wa wanawake katika usimamizi wa misitu na shughuli za kujiongezea kipato umewawezesha kupata uhuru wa kifedha. "Siku hizi hatuhitaji kuwaomba wanaume fedha kwa matumizi madogo madogo," alisema Bi. Hadija Manyagala, mkazi wa Lusane.


Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union

JINSI USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MISITU UNAVYOHIFADHI MAZINGIRA, KUIMARISHA UCHUMI NA KUBORESHA MAISHA YA JAMII



Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni, Bi. Ester Gama, akikabidhi mavazi na viatu kwa Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Kwakibuyu. Msaada huo umeongeza ufanisi wa wajumbe katika doria za misitu, kudhibiti uvamizi na uharibifu, na kuimarisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za misitu



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maliasili na Utalii

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA ..KWAKIBUYU..

JEDWALI

Imeandaliwa chini ya Kifungu 49 cha sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na Kanuni ya 3 ya Kanuni za Misitu 2004

Fomu Na. UDMA 1

Leseni Na.

LESENI YA KUVUNA MAZAO YA MISITU KATIKA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI 49015

Ofisi ya Kijiji cha ..KWAKIBUYU..

Leseni hii imetolewa kwa ..MOHAMED ANOUR AHMED.. wa S.L.P ..89..

kwa ajili ya kuvuna/kukusanya katika msitu wa hifadhi wa Kijiji cha ..KWAKIBUYU..

Msitu wa ..BOJO.. (mahali)

Maelezo, kiasi na thamani ya mazao ya misitu yameelezwa hapa chini:

Maelezo na kiasi wa mazao ya misitu (mita za ujazo (M³) wa miti, kilo za asali)	*Aina ya Mti/Miti*	*Kiwango cha Ushuru kwa Ujazo/ Idadi/ada Tshs*	*Thamani ya Mazao Tshs*
4000KGS(80GUNIA)	MIOMBO	12,500/=	1000,000/=
			1,000,000/=

Mapato/Ushuru wa jumla ya Tshs. 1,000,000/= kwa ajili ya Usimamizi Shirikishi wa Msitu umeshalipwa na mvunaji kwa Risiti Na. 025365 ya Tarehe 06/10/2026

Mvunaji pia amelipa/amefidia Kiasi cha Shs. ..... Kwa Risiti Na. .....

ya Tarehe .....

06/10/2026 — *Tarehe*

MWANAHAMISI H. MTUMBA — *Jina la Mweka Hazina Kamati ya Maliasili ya Kijiji*

Sahihi na Muhuri

MASHARTI

1. Leseni hii itadumu kwa muda wa siku 30 toka tarehe ya kutolewa
2. Leseni hii inaweza kuongezwa muda kwa masharti kwa kuandikia uongozi wa kijiji ndani ya kipindi cha siku 15 (kumi na tano) baada ya kulipa faini ya asilimia 20% (ishirini) juu ya thamani ya mapato ya leseni hii.
3. Mwenye leseni hana mamlaka juu ya majani na mizizi ya miti iliyovunwa
4. Hakuna uradishaji wa fedha zilizolipwa kwa mazingira ya miti/miti kuwa na ubovu wowote.
5. Leseni itarudishi miti ile tu iliyowekwa alama kwa ajili ya kuvunwa
6. Mwenye leseni atalipa mapato kamili kama ilivyopendekezwa na kijiji na/au faini kulingana na uharibifu kwa miti mingine au kukabiliana na hatua zingine za kisheria
7. Mazao yote ya misitu yataondelewa kabla ya muda wa leseni hii kuisha kwa hati halali ya usafirishaji (Transit Pass) toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya

Mpiga chapa .....

Picha: Uhifadhi unaozaa matunda. Leseni ya kuvuna mazao ya misitu katika Hifadhi ya Msitu wa Kijiji cha Kwakibuyu ni ushahidi wa uhifadhi wenye mafanikio, unaowezesha jamii kunufaika kiuchumi kupitia uvunaji endelevu wa misitu.



Mkaa endelevu, rafiki wa misitu! Magunia ya mkaa yaliyovunwa kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya usimamizi wa misitu ya jamii, yakionesha jinsi matumizi endelevu ya rasilimali za misitu yanavyoweza kuleta kipato huku yakichangia uhifadhi wa misitu.



Kuimarika kwa doria katika Kijiji cha Mseko kumesaidia kudhibiti utoroshaji wa mazao ya misitu. Kijiji kilikamata na kutaifisha magunia 83 ya mkaa uliozalishwa kiholela na kupata Shilingi 1,600,000 kupitia mnada wa mkaa huo.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union

VIKUNDI VYA KUWEKA NA KUKOPA (VSLA) VYAFUNGUA MILANGO YA FURSA WILAYANI PANGANI

Umoja na maendeleo! Kikundi cha Hiyari ya Moyo, Kwakibuyu, kimepongezwa kwa mchango wake katika kuimarisha usimamizi wa fedha na mshikamano wa jamii wakati wa ziara ya mtaalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.





Mwanahawa Rajabu, mkazi wa Kijiji cha Kwakibuyu, ametumia mkopo wa hisa kukuza biashara yake ya ushonaji, kununua friji na kuanzisha biashara ya vinywaji baridi, na hivyo kuongeza fursa za kipato

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Co-funded by the European Union

MITANDAO YA MJUMITA TANGA

Mitandao ya kijamii imekuwa chachu ya utatuzi wa migogoro na changamoto za usimamizi shirikishi wa misitu, ikiwezesha wajumbe kupaza sauti kuhusu masuala ya ardhi na misitu, ambapo baadhi tayari yamepatiwa ufumbuzi.



1

Bwana Mussa Waziri Kumbo, Mwenyekiti wa Mtandao wa HIMIMSA, akieleza changamoto za uhifadhi wa misitu katika kikao cha wajumbe wa MJUMITA na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi.

Bwana Sadick Mungia, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Lusane na mjumbe wa Mtandao wa UMIMALUMA, akieleza changamoto za uhifadhi wa misitu katika mkutano na wataalamu wa Wilaya ya Kilindi

2





3

Bwana Mfaume Hassan Mafaume, Katibu wa Mtandao wa MJUMIKWEKIGE, akitoa ufafanuzi kwani mgeni aliyetembelea banda la mradi kuhusu manufaa na changamoto za usimamizi wa misitu ya jamii katika Maonyesho ya Mwenge wa Uhuru, Handen

Wajumbe wa Mtandao wa SAMIMKWE wakijenga uelewa wa wananchi kuhusu sera, sheria na miongozo ya usimamizi wa



4

Wajumbe wa mitandao ya MJUMITA wamekuwa wakipaza sauti katika majukwaa ya kitaifa kuhusu changamoto za utekelezaji wa sheria na miongozo ya usimamizi wa misitu ya jamii. Bi. Kinish Said Hassan, Katibu wa Mtandao wa SAMIMKWE, akichangia katika Mkutano Mkuu wa 25 wa MJUMITA uliofanyika Tanga, Aprili 2026